

HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA KWS DAKATARI ERUSTUS KANGA KATIKA SIKU YA KUADHIMISHA LUGHA YA KISWAHILI ULIMWENGUNI

Waziri wa Utalii, Wanyama Pori na Turathi za Kitaifa, Mheshimiwa Peninah Malonza,

Katibu Mkuu katika Idara ya Serikali ya Wanyama Pori, Mheshimiwa Silvia Museiya,

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Huduma kwa Wanyama Pori KWS,

Mabibi na Mabwana – Hamjambo

Ni furaha yangu kuu kujumuika na nyinyi hapa leo tukiadhimisha siku ya lugha ya Kiswahili ulimwenguni.

Lugha hii ya Kiswahili inatambulika na kuzungumuzwa na takriban watu millioni mia mbili kote ulimwenguni. Hii ni haswa hapa Afrika Mashariki na sehemu zingine zikiwemo Ulaya, Marekani na Bara Asia.

Hapa Kenya, Kiswahili ndio lugha rasmi ya taifa. Vile vile, hutumika sana katika shughuli za kitalii na za uhifadhi wa wanyama pori na viumbwe vya baharini.

Wanyama pori wametumika katika methali na misemo mingi ya Kiswahili. Kwa mfano,

1. ‘Usione simba amenyeshewa ukadhania ni paka’
2. ‘Nyani haoni kundule’
3. ‘Siku ya nyani kufa miti yote huteleza’
4. ‘Njia mbili zilimushinda fisi.
5. ‘Wakaazi wa Pwani husema: Avumaye baharini papa kumbe wengi wapo’
6. ‘Simba mwenda pole ndiye mla nyama

Naomba Mheshimiwa Waziri uniruhusu niachie wananchi wenyewe watafakari maana na matumizi ya methali hizi.

Mwisho, nahimiza ma afisa wangu wanao tangamana na wananchi mashinani, kutumia lugha hii kuelimisha na kuendeleza mikakati ya uhifadhi wa wanyama pori na turathi za kitaifa.

Ahsanteni nyote kwa kunisikiliza na mungu awabariki.